## TAASISI YA UTAFITI WA WANYAMAPORI TANZANIA (TAWIRI)

## TAARIFA KWA UMMA

# Ugunduzi wa dawa ya kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka kwa binadamu kutokana na mimea inayotumika kwa tiba asili

Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), kutoka mwaka 2013 imekuwa ikifanya utafiti wa mimea inayotumika kwa tiba asili katika ukanda wa kaskazini mwa Tanzania. Utafiti huu umefanyika katika wilaya za Ngorongoro, Mbulu na Hanang kwa watu jamii ya Masai, Hadzabe, Datoga na Iraqw. Lengo la utafiti huu lilikuwa kufanya ugunduzi wa dawa na vipodozi kutokana na bioanuwai ya mimea inayotumika kwa tiba asili; na pia kubaini mimea inayotumika kwa tiba asili ambayo iko katika hatari ya kutoweka ili kuihifadhi katika bustani za mimea au ‘botanical garden’.

Kutokana na utafiti wa bioanuwai ya mimea inayotumika kwa tiba asili, watafiti wa TAWIRI wamepata HATAZA (PATENTS) tatu za ugunduzi wa dawa au vipodozi asili kama ifuatavyo;

i. Dawa ya kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka kwa kutumia mmea uitwao **Mporojo.** Mmea huu kwa kiingereza unaitwa **wormwood albizia**/ bitter false thorn, jina la kisayansi unaitwa ***Albizia anthelmintica***. Kimasai unaitwa **Ormuktan** na Wamasai wanatumia magome na mizizi yake kutibu minyoo, malaria na maumivu ya miguu, mgongo na misuli. Utafiti huu ulikwenda zaidi ya matumizi haya na kugundua uwezo wa mmea huu kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka. Hataza hii inaitwa ‘Composition for Hair Growth Stimulation or Hair Loss Prevention Using an Extract of *Albizia anthelmintica’.*

Teknolojia ya Hataza hii imetolewa (patent transfer) kwa kampuni ya **Winwik Enterprise co., ltd** ya Korea Kusini ambayo ni watengenezaji wa Kimataifa wa dawa na vipodozi. Tunaujulisha umma kuwa tayari kampuni hii imeshatengeneza dawa ya kuotesha nywele (**Albizia Hair Loss Care**) katika mfumo wa **Shampoo** (shampuu ya wanawake na wanaume), **Dawa** (Treatment), na **Mafuta** (Hair Essence Tonic). Dawa/ vipodozi hivi vitaanza kupatikana kwa bei ya jumla kwa mawakala na pia rejareja hivi karibuni. Utafiti wa namna ya kuotesha Mporojo (propagation) kwa ajili ya kilimo cha Mporojo umeanza ili kuzuia mmea huu kutoweka kutokana na uvunaji wa magome kutoka mimea iliyopo porini.

**Matumizi**: Dawa au vipodozi hivi vinatumika kuotesha nywele, kuboresha/ kuimarisha nywele (zisikatike, kuwa nyingi), kuzuia nywele kutoka (kuzuia kipara), au kuondoa kipara.

Aidha, kutokana na utafiti huu, Taasisi imepata hataza (Patent) nyingine mbili kutokana na bioanuwai ya mimea inayotumika kwa tiba asili ambazo ni;

i. Ugunduzi wa kipodozi cha **kung'arisha ngozi na kuondoa makunyanzi** kwa kutumia mmea wa **Mugufe.** Mmea huu kwa kiingereza unaitwa **Evergreen shrub/** blue bush cherry. Jina la kisayansi la mmea huu unaitwa ***Maerua edulis****.* Mmea huu kwa **Kidatoga unaitwa Ekwida** na jamii hii inatumia majani yake kutibu **minyoo, tumbo na ngili**. Utafiti huu ulikwenda zaidi ya matumizi haya na kugundua uwezo wa mmea huu kung'arisha ngozi na kuondoa makunyanzi. Hataza hii inaitwa 'Composition for skin-lightening and improving wrinkle using extract of *Maerua edulis'.*

Teknolojia ya hataza hii bado haijanunuliwa au kupewa kampuni yoyote, hivyo bado Taasisi na washirika wake wanaendelea kuitangaza ili kupata atakayeihitaji ili kutengeneza kipodozi cha kung'arisha ngozi na kuondoa makunyanzi.

ii. Dawa ya kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka kwa kutumia mmea uitwao **Chimbulei (Kigwala, Mphata).** Mmea huu kwa kiingereza unaitwa **Apple leat**/ broadlance-pod. Jina la kisayansi unaitwa *Lonchocarpus eriocalyx.* Mmea huu kwa **Kisonjo unaitwa Ekurehe** ambapo Wasonjo wanatumia magome na mizizi yake **kutibu kikohozi na mafua**. Utafiti huu ulikwenda zaidi ya matumizi haya na kugundua uwezo wa mmea huu kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka. Hataza hii inaitwa 'Composition for Hair Growth Stimulation or Hair Loss Prevention Using an Extract of *Lonchocarpus eriocalyx'.*

Teknolojia ya hataza hii bado haijapewa kampuni yoyote, hivyo bado Taasisi na washirika wake wanaendelea kuitangaza ili kupata atakayeihitaji ili kutengeneza dawa ya kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka.

Watafiti walioshiriki katika utafiti, ugunduzi na Hataza hizi tatu kutoka TAWIRI ni Dkt. Julius Keyyu, Dkt. Bukombe John na Dkt. Angela Mwakatobe. Watafiti kutoka Taasisi nyingine walioshiriki ni kutoka Taasisi ya Bioanuwai ya Korea Kusini (NIBR) na Taasisi ya Tiba Asili Tanzania (ITM).


ALBIZIA
[ SCALP SKINCARE LAB ]
HAIR LOSS CARE
SHAMPOO
MAN
WOMAN
TREATMENT
HAIR ESSENCE TONIC
shampoo, treatment, etc.


ALBIZIA
SHAMPOO
MAN
Galaxy S23 Ultra


ALBIZIA
SHAMPOO
WOMAN
Galaxy S23 Ultra

**AHSANTENI**